

# **ADABU ZA SOKONI NA NJIANI**

Kimeandikwa na:  
**Jumuia ya Maarifa na Utamaduni wa Kiislamu**

Kimetarjumiwa na:  
**Amiri Mussa Kea**

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:  
AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 512 - 35 - 5**

Kimeandikwa na:  
**Jumuia ya Maarifa na Utamaduni wa Kiislamu**

Kimetarjumiwa na:  
**Amiri Mussa Ke a**

Kimepangwa katika Kompyuta na:  
**Hajat Pili Rajab**

Toleo la kwanza: Julai, 2009  
**Nakala: 1000**

**Kimetolewa na kuchapishwa na:  
Alitrah Foundation**

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: [www.alitrah.org](http://www.alitrah.org)

Katika mtandao: [www.alitrah.info](http://www.alitrah.info)

**ترجمة**  
**أداب السوق والطريق**  
**تأليف**  
١ عدد ونشر جمعية المعرفة الإسلامية الثقافية  
من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

## **Adabu za Sokoni na Njiani**

---

# **Yaliyomo**

<b>Utangulizi.....</b>	2
Adabu za Njiani.....	2

<b>Maelezo.....</b>	3
---------------------	---

1. Kuhifadhi usafi Njiani.....	3
2. Kupanua Njia.....	5
3. Kuijepusha na yale ambayo huondoa Murua.....	7
4. Kuwashudumia Wasafiri.....	8

<b>Adabu za Kutembea.....</b>	9
-------------------------------	---

1. Unyenyekevu katika Kutembea.....	10
2. Upole katika Uendaji.....	11
3. Kutosukuma wengine (vikumbo).....	12

<b>Mwanamke atembee wapi?.....</b>	13
------------------------------------	----


Adabu za Sokoni.....	13
----------------------	----

<b>Utangulizi.....</b>	14
------------------------	----

Soko ni mahala pa utukufu wa Muumini.....	15
Soko la Mashetani.....	16

<b>Mawaidha ya Amirul-Mu'minin kwa watu wa sokoni.....</b>	16
--	----

1. Ukweli katika soko la Waislamu.....	18
--	----



## **Adabu za Sokoni na Njiani**

---

2. Tutaamiliana na nani sokoni.....	19
3. Kumtaja Mwenyezi Mungu sokoni.....	20
4. Mipaka katika yale unayonunua.....	22

<b>Muuza</b> ji Sokoni.....	22
-----------------------------	----

Sehemu ya kuuza Sokoni.....	23
-----------------------------	----

<b>Adabu</b> za Muuzaji.....	24
------------------------------	----

1. Dua Sokoni.....	24
2. Uwazi katika Uuzaji na Ununuzi.....	26
3. Biashara isiwapumbaze kuhusiana na Swala.....	26
4. Kutoapa katika Uuzaji.....	27



## NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kii twacho, *Aadaabu 's-Sawq wa 't-Tariiq*. Sisi tumekiita, *Adabu za Sokoni na Njiani*. Kitabu hiki kimeandikwa na Jumuia ya Maarifa na Utamaduni wa Kiislamu.

Inafahamika vizuri kwamba kwa vile Uislamu ni dini na ni mfumo wa maisha, hivyo, haukuacha jambo lolote linahusu maisha ya mwanadamu. Uislamu umetengeneza kanuni, sheria na adabu zinazohusu kila suala la mwanadamu. Soko na njia ni maeneo ambayo watu wa kila aina huyatumia katika maisha yao ya kila siku. Katika muktadha huu, soko ni kuanzia maduka madogo ya mitaani, maduka makubwa (*supermarkets*), na masoko ya kitaifa na kimataifa. Njia katika muktadha huu ni kuanzia njia za kawaiida wanazotumia watu (za miguu), barabara za magari, reli, usafiri wa majini na angani, kitaifa na kimataifa. Kwa hiyo, Uislamu umeweka kanuni, sheria na adabu kwa ajili ya matumizi ya watu katika maeneo hayo ili kulinda haki ya kila mtu.

Mwandishi wa kitabu hiki ameelezea kanuni, sheria na adabu zinazotumika katika maeneo hayo kwa mujibu wa mafundisho ya Kiiislamu ambayo ni kutoka katika Qur'ani Tukufu na Sunna.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, kwani kinagusa harakati za maisha ya watu ya kila siku. Tunakitoa kwa lugha ya Kiswahili kwa malengo yetu yaleyale ya ku wahudumia wasomaji wetu wazungumzaji wa Kiswahili ili wapate kuongeza elimu yao ya dini na ya kijamii kwa ujumla.


Tunamshukuru ndugu yetu, Sheikh Amir Musa Kea kwa kukubali kukitar-jumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.




**Mchapishaji:**

Al-Itrah Foundation

S. L. P. 19701

Dar-es-Salaam, Tanzania.





H

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

## Adabu za Sokoni na Njiani

# Utangulizi

Kila sifa njema anastahiki Mola wa viumbe, kisha rehema na amani zimfikie aliyetumwa kwa watu wote Abul-Qaasim Mtume Muhammad {s.a.w.w} na Aali zake watoharifu.

Sehemu za umma ambazo watu wote hushirikiana katika uislamu zina hukumu na adabu zake, kwa hivyo ni juu ya kila binadamu mwenye imani kuzichunga na kutokwenda kinyume nazo, hana haki yoyote ya kujipendelea na kuzitumia yeye binafsi, na sio miliki ya mtu fulani, kuwa yeye ndiye anayestahili na kujilimbikizia yeye, vile vile azitumie namna apendavyo, mfano wa sehemu hizo ni njia na soko, kwa hakika vitu hivyo watu wote wana haki sawa, kwa hivyo hapa linakuja swali: Ni adabu zipi ambazo Uislamu umeziweka kuhusiana na sehemu hizo na ambazo umetutaka sisi tuzifuate?

Tutaeleza katika kitabu hiki kuhusiana na adabu ambazo zimepokewa kutoka kwa Ahlul-Bayt {a.s} walio maasumu na watoharifu katika sehemu hizi mbili sokoni na njiani, huenda akatuwezesha Mwenyezi Mungu {a.j} kufuata adabu hizo ambazo ni sira na nyendo za mawalii wake, kwa hakika Yeye ni Msikifu Mwitikia maombi.

## ADABU ZA NJIANI

Mtume {s.a.w.w} amesema:

"دخل عبد الجنة بغضن من شوك كان على طريق المسلمين فأماته عنه"

"Mja atakuwa ameingia peponi kwa kuondoa tawi la miiba lililokuwa kwenye njia ya waislamu".

## Adabu za Sokoni na Njiani

### Maelezo:

Hakika njia ambazo binadamu hupita zina adabu nyingi ambazo Uislamu umetilia umuhimu sana, umezibainisha na kuzisisitiza zizingatiwe na zifu-atwe, yapo maandiko mengi ya kisheria kuhusiana na hilo...

Kwa hivyo mwenye kuchunga adabu za njiani kwa hakika humuepusha na ubinafsi, kujipendelea ili aishi katika jamii yote kwa upendo mkubwa na kupenda heri kwa kila mpita njia, naye katika wakati huo huo huonyesha sura na mtazamo mzuri katika jamii anayoishi...

Ni dhahiri shahiri kwamba mtu ye yole yule ambaye huingia katika jamii yoyote ile, kitu cha kwanza ambacho hukiona ni barabara, mazingira yanayoizunguka, utaratibu na mpangilio wake, hali kadhalika tabia za watembeao na wavukao barabara, kwani hayo yote yatamfichulia tabia za jamii hiyo na maendeleo ya watu wake.

Kwa mantiki hiyo tunaona mkazo na msisitizo wa Uislamu juu ya kadhia hiyo uliolezwa kwa mrefu na mapana, kwa hakika njia au barabara ni dirisha ambalo wachunguzi huangalia dhahiri ya maisha ya waislamu wote, na wanachukua kwayo dhana kutokana na njia ya maisha yao, na wanafichua kutokana na hayo matendo yanayotokana na mtu, kwani hud-hihirisha utamaduni aliokuwa nao ... ni adabu gani hizo ambazo uislamu umesisitiza zichungwe na zifanyiwe kazi?

Zipo adabu nyingi sana ambazo zimeelezwa kuhusiana na kadhia hiyo, hapa tunataja baadhi ya hizo:

### 1. KUIWEKA NJIA KATIKA HALI YA USIFI

Uislamu umetilia umuhimu mkubwa suala la usafi, na kwa hivyo Uislamu umeweka adabu ili kuhifadhi suala la usafi katika yale ambayo yanafungamana na maisha ya binadamu muumini anayeishi katika jamii husika, ama

## Adabu za Sokoni na Njiani

yale yanayofungamana na nafsi yake au yale ambayo yanahuksiana na mavazi yake, nyumba yake na njia anayopita.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Mtume {s.a.w.w} amesema: “Mja mbaya ni yule mchafu”<sup>1</sup> Vilevile {s.a.w.w} amesema: “Wameangamia watu wachafu”<sup>2</sup>

Kama vile yapo maangamio katika upande wa kimaada namna ambayo huleta na kusababisha maradhi pamoja na maisha mbaya, vivyo hivyo huathiri binadamu katika upande wa kiroho.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Mtume {s.a.w.w} amesema: “Hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri humpenda mtu mzuri na msafi na anayependa usafi”<sup>3</sup>

Kwa hivyo kama tulivyosema hapo kabla kwamba athari za usafi hazihusiani wala kuishia tu upande wa kimaada bali huvuka na huwa ni sababu mionganoni mwa sababu za kupata upendo wa Mungu.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Ridha {s.a} amesema: “Mionganoni mwa tabia za mitume ni usafi”<sup>4</sup>

Hadithi hizo zinajulisha juu ya mambo mawili; huashiria usafi na kwamba ulikuwa ni jambo la kudumu, aidha ni mfumo wa maisha wa Mitume {a.s}, na ndiyo nyendo walizojulikana kwa watu, vilevile hutoa ishara kwamba usafi ni mionganoni mwa mambo ya kitabia, kwa hivyo usafi ni jambo la dhahiri ambalo hupelekeaa athari zake katika mambo ya batini.

<sup>1</sup> *Miizanul-Hikma* Hadithi 20317.

<sup>2</sup> *Miizanul-Hikma* Hadithi 20318.

<sup>3</sup> *Miizanul-Hikma* Hadithi 20314.

<sup>4</sup> *Miizanul-Hikma*, Hadithi 20330.

## Adabu za Sokoni na Njiani

---

Ewe mpendwa muumini iwapo unataka kutembea njiani kwa utaratibi wa manabii na unapenda usifike kwa tabia njema basi jua kwamba usafi na kuwa katika nyendo za manabii ni moja ya tabia ambazo yakupasa kushikamana nazo.

### **2. UPANUAJI WA NJIA**

Hakika njia kwa msingi imewekwa ili kila mpita njia aitumie na afaidike nayo, kwa hivyo ni haki ya watu wote wala haimuhusu mtu mmoja pekee, kwa mantiki hiyo kuwabania wao njia ni kupora haki yao, kwa ajili hiyo inampasa kila mpita njia kuwapa nafasi ya njia wengine, wala asisimame njiani katika hali ambayo atafanya njia iwe finyu.

Imepokewa kutoka kwa Amirul-Mu'miniina {a.s} katika usia wake kwa Imam Hasan {a.s} amesema: "Jiepushe kukaa njiani"<sup>5</sup>

Pamoja na kuwepo msongamano mkubwa wa magari njiani, mara nyingi tumekuwa tukikumbana na masuala mbalimbali yanayotokea njiani ikiwa ni pamoja na kuwabania watu njia, hasa hasa mijini kuna misongamano mingi, kwa hivyo ni juu yako kuchukua tahadhari pamoja na kujiepusha kuegesha gari yako katika sehemu ambayo utawabania watu njia, wala huheshimu haki ya watu kupita kwa uhuru. Na jaribu kujiepusha kuzungumza na mwagine kuitia dirisha la gari yako ikiwa imesimama katikati ya barabara, vilevile jaribu kutoshusha bidhaa yako mahsus kwenye njia ambayo imeandaliwa kwa ajili ya wapitaji... na vizuizi vinginevyo ambavyo hubana njia na huleta msongamano kwa wapitaji, kwa mantiki hiyo ndiyo maana tumeamrishwa kuviondoa.

Vivyo hivyo usiweke kile ambacho huzuia harakati za upitaji bali ni katika mambo ya lazima kuondoa kitu ambacho kwa njia moja au nyigine kitawaudhi na kuwasumbua wapitaji, Mwenyezi Mungu {a.j} amemuan-

<sup>5</sup> *Al-Amaal*, uk. 222 cha Sheikh Mufiid.

## Adabu za Sokoni na Njiani

dalia malipo makubwa yule ambaye hujipamba na tabia hii ya kuwafanya wepesi wapita njia kama ilivyokuja katika hadithi tukufu.

Bwana Mtume {s.a.w.w} amesema: “Mja ameingia peponi kwa kuondoa tawi la miba lililo kwenye njia ya waislamu”<sup>6</sup>

Na katika hadithi nyingine amesema: “Ni juu ya kila Mwislamu kutoa swadaka kila siku” ikasemwa: Ni nani atakayeweza hilo? Akasema: “Kuondoa kitu njiani ambacho huleta madhara kwa watu pia ni swadaka”<sup>7</sup>

Bali ametuamrisha tutengeneze njia na kuisafisha, na malipo yake huwa ni kuondolewa adhabu, kama ilivyokuja katika baadhi ya hadithi tukufu, Mtume {s.a.w.w} amesema: “Isa bin Maryam {a.s} alipita katika kaburi ambalo aliyekuwemo kaburini alikuwa akiadhidiwa, kisha akapita mwaka uliyofuata hakuona akiadhidiwa akasema: Ee Mola wangu nimepita kwenye kaburi hili mwaka uliyopita alikuwa akiadhidiwa na nimepita mwaka huu haadhibiwi kulikoni? Mwenyezi Mungu {a.j} akampa wahyi: Ewe Roho wa Mwenyezi Mungu, mtu huyo aliacha mtoto mwema akasafisha njia na akampa hifadhi yatima basi nikamsamehe yeye kutohana na matendo ya mwanawewe”<sup>8</sup>

Chunguza thamani ya tendo hili ambalo baraka zake zimemfikia baba aliyekufa kutoka kwa mwanawewe na ikawa sababu ya kuondolewa adhabu!

Na kutohana na yale yaliyotangulia tunajua kwamba hakika muumini hubeba masumbu ya watu hata mawe, kutoka njiani mwao na vipande vyaa chupa kutoka njiani kuwakinga wadogo wao...

<sup>6</sup> *Khiswatu*, Juz. 1, uk. 32 Hadithi 111.

<sup>7</sup> *Mustadrakul-Wasa'il*, Juz. 2, uk. 402 mlango 19 Hadithi 6.

<sup>8</sup> *Amaal*, uk. 512 Majlis ya 77 Hadithi 8.

## Adabu za Sokoni na Njiani

### 3. KUJIEPUSHA NA YALE AMBAYO HUENDA KINYUME NA MURUA

Kuna mambo mengi ambayo hayanasibiani na utu na mazoea, na Mwenyezi Mungu {a.j} anamtaka muumini silika zake ziende sanjari na jamii, kwa hivyo sheria tukufu zimetilia mkazo juu ya mambo kadhaa ambayo yampasa muumini afanye inavyostahili, na ajiepushe na baadhi ya mambo katika sehemu za uma hasa hasa njiani na barabarani, namna ambayo huzingatiwa kitendo chake hicho njiani huenda kinyume na murua.

Miongoni mwa mambo hayo ni:

**\* Kula Chakula:**

Jambo hilo ni makuruhu kama ilivvyokuja katika sheria. Imepokewa kuto-ka kwa Imam Kadhim {a.s} kwamba siku moja aliulizwa kuhusiana na mtu wa hali ya chini kwa tabia? akasema: “Ni yule anayekula masokoni”.

**\* Kutafuna Ubani:**

Ni katika yale mambo ambayo yanayotweza. Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Baqir {a.s} amesema: “... Kuvurumisha vijiwe na kutafuna ubani katika vikao na kukaa katikati ya njia ni katika matendo ya watu wa Lut”<sup>9</sup>

**\* Kucheka kwa kutoa sauti kubwa:**

Ahlul-Bayt {a.s} wameeleza kuwa kazi hiyo ni miongoni mwa kazi za Shetani, ipo hadithi iliyopokewa kutoka kwa Abu Abdullah {a.s} amese-

<sup>9</sup> *Man la Yahdhuruhul-Faqih*, Juz. 1, uk. 260.

## Adabu za Sokoni na Njiani

---

ma: "Kicheko cha sauti kinatokana na Shetani"<sup>10</sup>

Kwa hakika yampasa mtu kuacha hilo ili utu, shakhsiya na haiba ya muumini ibakie, aidha ipo hadithi nyingine kutoka kwake {a.s} amesema: "Kucheka sana kunaondoa maji ya uso {murua}"<sup>11</sup>

### **4. Kuwahudumia Wasafiri:**

Uislamu umetilia mkazo juu ya kuwahudumia watu na kuwakidhia haja zao, na binadamu akiwa safarini haja zake huzidi za kimaada na za kiroho, nayo ni natija ya mchoko wa kimwili ambao hukumbana nao akiwa safarini na mchoko wa kiroho ambao huenda ukamtokea yeze hasahasa kutokana na kuwa na mwenzi safarini asiyelingana.

Kwa hivyo safari huzingatiwa kuwa ni mionganini mwa hali za kipekee ambazo binadamu huhitaji mkono ambao utamshika na kumuondolea na kufuta taabu za njiani kwenye paji lake la uso, kwa hivyo tunakuta hadithi chungu nzima zinazotuelekeza kwa watu hawa na kutuhimiza tuwasaidie kwa kile kiwezekanacho ili kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu {a.j} hasa katika safari ndefu. Mwenyezi Mungu {a.j} ameratibu ujira mkubwa zaidi kwa ajili ya kazi hii kuliko anavyofikiri binadamu.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Mtume {s.a.w.w} amesema: "Mwenye kutengeneza sehemu ya mapumziko kwa ajili ya mpita njia, Mwenyezi Mungu atamfufua mtu huyo siku ya Qiyama katika ulodi kutokana na lulu na johari na uso wake ukitoa mwanga wa nuru kwa watu waliokusanyika itakayofika hadi katika kuba la Ibrahim al' Khalil {a.s}, hapo waliokusanyika watasema: "Huyu ni Malaika mionganini mwa Malaika, hatujamuona mfano wake katu, na wataingia katika uombezi wake watu wa peponi maelfu arobaini ya watu. Na mwenye kuchimba kisima cha maji hadi maji yakatoka, kisha maji hayo akawapatia waislamu atapata yeze

<sup>10</sup> *Kaafi*, Juz. 2, uk. 664.

<sup>11</sup> *Kaafi*, Juz. 2, uk. 664.

## Adabu za Sokoni na Njiani

malipo kama vile yule aliyechukua udhuu na akaswali na atapata ujira sawa na idadi ya kila unywele mmoja wa mwenye kunywa maji hayo mionganoni mwa binadamu, mifugo, wanyama wenyewe kushambulia au ndege, na sawa na kuwaacha huru watu watumwa elfu, na attingia katika hodhi ya Quddus Siku ya Qiyama, na wataingia katika uombezi wake watu sawa na idadi ya nyota” ikasemwa: Ee Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ni nini hiyo hodhi ya Quddus? Akasema: “Ni hodhi yangu ni hodhi yangu<sup>12</sup> mara tatu”.

Na katika hadithi nyingine {s.a.w.w} amesema: “Mwenye kuchimba kisima au hodhi jangwani ataswaliwa na Malaika wa mbinguni, na atapata malipo kwa kila atakayekunyuwa mionganoni mwa binadamu, ndege au wanyama maelfu ya wema yenye kutakabaliwa na shingo elfu mionganoni mwa kizazi cha Ismail na ngamia elfu, na itakuwa ni haki ya Mwenyezi Mungu kumuingiza mtu huyo katika Boma la Qudus”<sup>13</sup>

## ADABU ZA KUTEMBEA

Mwenyezi Mungu {a.j} anasema:

﴿وَلَا تُصْعِرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ

مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿١٨﴾

**“Wala usigeuze mashavu yako kuwabeuwa watu, wala usitembee kati-ka nchi kwa maringo, hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivu-naye, ajifaharishaye” (31:18)**

Miongoni mwa mambo ambayo sheria ya kiislamu imetilia mkazo mahsusini suala la namna ya utembeaji njiani, hali ambayo yamkini kwa mtembeaji

<sup>12</sup> *Mir'atul-Kamaal*, Juz. 2, uk. 347-348.

<sup>13</sup> *Mustadrakul-Wasa'il*, juz. 2, uk. 402 mlango 20 Hadithi 1.

## Adabu za Sokoni na Njiani

kupindua hatua za mtu za kitabia na hali zake za kinafsi na kubainisha sehemu muhimu ya utu wake, kutokana na yale ambayo huyaficha lakimi hufichuliwa na silika hizi za kawaida ambazo hudhihiri baadhi yake katika utembeaji wake, kwa hivyo Uislamu umetilia mkazo hilo kwa kuondoa uchafu katika njia hizi, basi ukauwekea utembeaji adabu ili mwislamu azifuate kwazo.

### 1. Unyenyekevu katika Utembeaji

Mwenyezi Mungu {a.j} amekataza utembeaji ambao hudhihirisha kwamba binadamu ana tabia ya kiburi na kijikweza kwa wengine, na tabia ya mtu kujikweza kwa wenzake ni jambo ambalo limekatazwa na Mola Manani katika Kitabu Chake kitukufu kuhusiana na utembeaji wa maringo na kuifaharisha, bali inambidi mtu asiwafanyie watu jeuri pale aliposema:

﴿ وَلَا تُصْعِرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّ اللَّهَ لَا تَنْهِبُ كُلَّ ﴾

مُحَمَّدٌ فَخُورٌ ﴿١٨﴾

“Wala usiwabeuwe watu, wala usitembee katika nchi kwa maringo, hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye”  
31:18

Kugeuza mashavu: Yaani Binadamu kuuzungusha uso wake mbali na anayeongea naye kwa namna inayomjulisha hamtilii manani yeze na mazungumzo yake.

Na kufanya maringo katika kwenda ni mtu kuinua mabega yake wakati wa kwenda moja juu, kudhihirisha nguvu na majigambo na kuinua kichwa chake kuonesha makuu na kuwa yu tofauti na wengine.

Mtume {s.a.w.w} amemwelezea mtu ambaye anatembea kwa majivuno kuwa ni mwendawazimu. Imepokewa hadithi kutoka kwa Mtume

## Adabu za Sokoni na Njiani

{s.a.w.w} amesema: "Hakika mwendawazimu ni mwenye kujifaharisha katika utembeaji wake, mwenye kuangalia kwapa zake, mwenye kutingisha pande zake mbili kwa mabega yake, basi huyo ndiyo mwenda wazimu"<sup>14</sup>

Hadi ardhi inamlaani yule ambaye anaitembea kwa hali hiyo, imekuja katika hadithi tukufu kwamba bwana Mtume {s.a.w.w} amesema: "Mwenye kutembea juu ya ardhi kwa maringo na kujifaharisha hulaaniwa na ardhi na yule aliye chini yake na juu yake"<sup>15</sup>

Kwa hivyo ni juu ya kila mtu awe ni katika tabia yake hali akitembea njiani awe mnyenyeketu katika utembeaji wake. kwa kuwa unyenyeketu katika mwendo ni tabia ya wachamungu.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Amirul-Mu'minin ameeleza sifa za wachamungu kwa kusema: "Mavazi yao ni wastani na utembeaji wao ni wa unyeyekevu"<sup>16</sup> **وَمُلْبِسُهُمُ الْأَقْتَصَادُ وَمُشَيْهُمُ التَّوَاضُعُ**

## 2. Upole katika utembeaji

Miongoni mwa mambo ambayo yamehimizwa na hadithi mbalimbali za maasumiin ni binadamu atembee kwa upole na apambike kwa utulivu, na aache yale ambayo yanasababisha kwa njia moja au nyingine kuondoa utu na heshima yake, hasa hasa ukimbiaji wa kasi isipokuwa katika hali ya dharura ambayo itamsababisha kufanya hayo.

<sup>14</sup> Biharul-Anwar, Juz. 76, uk. 57.

<sup>15</sup> Thawabul-A'maal wa Amali, cha Swaduq amenukuu kutoka Tafsir Nuru Thaqalayni.

<sup>16</sup> Nahjul-Balaghah, hutuba ya 184, inajulikana sana kwa jina la hutuba ya Wachamungu.

## Adabu za Sokoni na Njiani

Imepokewa kutoka kwa Mtume {s.a.w.w} amesema: “Utembeaji wa haraka huondoa hadhi ya mtu”<sup>17</sup>

Kwa hivyo tunawaona katika sira ya bwana Mtume {s.a..w.w} na Ahlul-Bayt wake walikuwa wakitembea kwa utulivu na upole, na pindi tunapozitupia macho hadithi zinazoeleza sifa zao tunazikuta zinaeleza namna ulivyokuwa utembeaji wao wa upole, na katika wasifu wa Imam Zaynul-Abidiina {a.s} imeelezwa kwamba: “Hakika yeye alipokuwa akitembea mkono wake ulikuwa hauvuki paja lake wala hakulemeza mkono wake na alikuwa mtulivu na mnyenyeketu”<sup>18</sup>

### **3. Kutosukumana (Kutopiga vikumbo)**

Usukumaji huenda wanaume wakawafanya wanawake na pia ikawa kinyume na hivyo, mambo yote mawili hayafai, kwa hivyo ni juu ya mwanamke ajichunge kusukumana {au kupigana vikumbo} na wanaume, vivyo hivyo kwa mwanaume ajiepushe iwezekanavyo kufanya yale ambayo kwa njia moja au nyingine yatamfanya apige vikumbo hasa hasa katika njia finyu au yenye msongamano.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Swadiq {a.s} amesema: Amirul-Mu’miniina amesema: “Enyi watu wa Iraq nimepata habari kwamba wanawake wenu hupigana vikumbo na wanaume njiani, hamuoni haya?”<sup>19</sup>

Na katika hadithi nyingine amesema: “Ama hamuoni haya wala hamuwaonei wivu wanawake wenu, wanatoka kwenda masokoni na husongamana na wavimba misuli<sup>20</sup>...”<sup>21</sup>

<sup>17</sup> *Miizanul-Hikma*, Juz. 7, uk. 2908.

<sup>18</sup> *Miizanul-Hikma*, Juz. 7, uk. 2908.

<sup>19</sup> *Wasa'il Shi'iah*, Juz. 2, uk. 235.

<sup>20</sup> Ni mwanaume mwenye nguvu, na ikasemwa kuwa ni kila mwenye ndevu.

<sup>21</sup> *Kaafi*, Juz. 5, uk. 518.

## Adabu za Sokoni na Njiani

### Wanawake watembee wapi?

Hakika uislamu kulingana na sheria zake zote unataka kumlinda mwanamke kupatwa na ubaya kutoka kwa wengine, kwa hivyo umemwekea yeye adabu mahsusizi za utembeaji njiani, nayo ni asitembee katikati ya njia bali atembee pembezoni ili asigongane na wanaume na kutambulika na wapumbavu mionganoni mwao.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Mtume {s.a.w.w} amesema: “Wanawake hawapaswi kutembea katikati ya njia lakini wawe wanatembea upande wa ukuta wa njiani”<sup>22</sup>

Na imepokewa hadithi kutoka kwa Abul Hasan {a.s} amesema: “Haimpasi mwanamke kutembea katikati ya njia, lakini yeye atembee pembezoni mwa ukuta”<sup>23</sup>

## ADABU ZA SOKONI

Imepokewa hadithi kutoka kwa Amirul-Mu'minin Ali bin Abi Twalib {a.s} amesema:

**”ايها التجار قدموا الاستخاره و تبركوا بالسهولة و اقتربوا من المبتعين و تزينوا بالحلم و تناهوا عن اليمين و جانبوا الكذب و تجافوا عن الظلم و انصفوا المظلومين ولا تقربوا الربا وأوفوا الكيل والميزان ولا تبخسوا الناس أشيائهم ولا تعثروا في الأرض مفسدين“**

“Enyi wafanyabiashara, muombeni ushauri Mwenyezi Mungu, na mtabaruku kwa wepesi, kuweni karibu na wanunuzi, jipambeni kwa upole, acheni viapo, jiepusheni na uongo, na acheni dhuluma, fanyeni insafu kwa waliodhulumiwa, wala msiikaribie riba, tekelezeni vipimo na mizani, msipunguze vitu vya watu na wala msiwe wafisadi katika ardhi”.

<sup>22</sup> *Kaafi*, Juz. 5, uk. 518.

<sup>23</sup> *Man la Yahdhuruhul-Faqiih*, Juz. 3, uk. 561.

## Adabu za Sokoni na Njiani

---

# Utangulizi

Hakika kupanga mambo ya watu katika maisha yao huhitaji kuweka kanuni inayoheshimu humo nyanja zote, namna na vipengele vyote, na jambo hili la kutilia umuhimu nyanja zote halimo katika uwezo wa kanuni inayowekwa na wanadamu, kwani hata ikitimiza kitu bado haiachi kuwa na mapungufu na dhuluma katika mambo mengi. Na hupungukiwa na jambo lingine nalo ni kutotilia umuhimu kwa kadhia ya mtu binafsi, na wala haiangalii uhusiano wa watu kitabia ili kuweka mpangilio. Hiyo ni kinyume na sheria na mpango wake, yenyewe ukiachia mbali kutengeneza kwake nidhamu ya mahusiano ya kiujumla, pia hujumuisha mambo mengi yanayohusu adabu ambazo mahala pake ni ndani ya nafsi ya binadamu, kwani humlea katika kuimarisha nguzo za akhlaq katika nafsi yake ili ziakis-isi uzuri na wema, na kwenda sanjari pindi anapokutana na wengine. Na suala la soko ni suala ambalo lina umuhimu mkubwa kutokana na soko kuwa ni:

**Mosi:** Kituo cha mji na mahala pa shughuli za kiuchumi.

**Pili:** Moja ya sehemu ambazo watu wengi hukutana, na kutokana na hali ya kukutana watu sehemu moja ni kawaida hutokea mgongano kati ya mtu na mwingine, na huenda kutokuwepo utaratibu na mipangilio au katazo la ndani kukasababisha matatizo mengi, ambayo hutokea na huleta sura iliyoko kinyume, na hivyo kuharibu uhusiano wa kidugu wa wanajamii moja, ambao Uislamu kuititia mipango na mikakati yake mbalimbali unahangai-ka wakati wote kwa lengo la kuuhifadhi ili jamii iwe kitu kimoja yenye kushirikiana baina yake.

Kwa hivyo tunajaribu katika kurasa hizi kueleza baadhi ya mambo yaliyokuja katika sheria ya kiislamu mionganini mwa mafundisho na adabu ambazo yamkini mtu kuzizingatia hizo masokoni, na tunamwomba Mwenyezi Mungu {a.j} atusaidie katika kumtii Yeye katika kila mambo yetu hakika Yeye ni Msikivu Mwenye kujibu.

## Adabu za Sokoni na Njiani

### SOKO NI MAHALA PA UTUKUFU WA MUUMINI

Ili jambo liwe lenye kusifiwa na kupendeza hapana budi liwe na kiwango kizuri cha ukamilifu, kwa hivyo soko lenye kusifika kwa sifa nzuri ni lazima lienee mambo kadhaa, kama ilivyoelezwa na hadithi kwamba ni maha-la patuku kwa yule mwenye kujishungulisha humo, Mulla bin Khunis ame-pokea kwamba Imam Swadiq {a.s} siku moja alimuona hakuenda sokoni, akamwambia: “Kesho nenda katika utukufu wako”<sup>24</sup>

Iweje sokoni pawe ni sehemu ya utukufu kwa muumini? Ni kazi inapokuwa ina lengo la halali na linalokubalika kisheria, aidha hakuna udangayifu, vitimbi na nia mbaya, binadamu anafanya hivyo ili kutafuta kipato kwa ajili ya familia yake katika huwapatia chakula wao, wala mtu asifanye udanganyifu kwa wanunuzi ili kujipatia kipato kwa njia ya hara-ka, yampasa kuendelea katika kuchuma kwa njia ya halali kwa kutooka na jasho la uso kwa lengo la kijikurubisha kwa Mwenyezi Mungu {a.j} kwa kazi yake aifanyayo, kazi yake huwa ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu bali huwa ni mfano wa kuigwa wa nyendo nzuri na nafsi safi, mtu huyu mweye mtazamo na nia kama hiyo, bila shaka ndiye ambaye soko kwake ni maha-la patukufu, na anakuwa uthibitisho wa maneno ya Imam Swadiq {a.s} ali-posema: “Mtafuta riziki kwa ajili ya familia yake ni kama vile mwenye kupigana vita katika dini ya Mwenyezi Mungu.”<sup>25</sup>

<sup>24</sup> *Man la Yahdhuruhul-Faqiih*, Juz. 3, uk. 192.

<sup>25</sup> *Kaafi*, Juz. 5, uk. 88.

## **Adabu za Sokoni na Njiani**

### **SOKO LA MASHETANI**

Mkabala na hadithi hizo ambazo zinalezea soko kwamba ni mahala patukufu kwa muumini tunazikuta hadithi zingine zinazoliezea soko kwa aina nyigine kuwa ni mahala pa shetani.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Swadiq {a.s} amesema: “Sehemu mbaya katika ardhi ni masokoni, napo ni mahala pa Ibilisi, huenda kwa bendera yake, hunyanya kiti chake na hueneza kizazi chake...”.

Ipi sababu ya hivyo? Imam {a.s} anaendelea kueleza: “...Yupo mwenye kupunguza katika kipimo chake, au mwenye kupunguza katika mzani, au mwizi katika dhiraa au mwongo katika biashara yake...”<sup>26</sup>

Kwa hivyo wewe wapigwa na butwaa, hivi iweje soko liwe na sifa hizo! Na sio jambo la ajabu soko kuwa ni mamlaka ya Ibilisi kwani hapo hufanywa mambo hayo ya maasi ambayo hufungamana na haki za watu, ambayo Mwenyezi Mungu {a.j} hasamehi kwa kutubia pekee, bali yahitaji kupata nsamaha toka kwa yule ambaye mali yake imeibiwa au kafanyiwa udanganyifu katika biashara husika.

### **MAWAIDHA YA AMIRUL-MU’MININ {A.S} KWA WATU WA SOKONI**

Ili mambo yasifike katika kiwango cha chini mionganii mwa tabia zisizofaa, Amirul-Mu’mimin {a.s} ana shauku kuwapa waadhi watu wa sokoni kama ilivyokuwa ada yake kuhifadhi na kulinda mambo yote ya kijamii.

<sup>26</sup> *Miizanul-Hikma*, Hadithi 9042.

## Adabu za Sokoni na Njiani

Alikuwa Imam Ali {a.s} akienda sokoni akibeba mjeledi ili kumchapia kila ambaye anawafanya udanganyifu waislamu, na waliokuwa wakijaribu kuwaibia wanunu<sup>27</sup> wa biashara zao, kisha alikuwa akisimama baina ya wafanya biashara akiwapa mawaidha akisema: “Enyi wafanyabiashara mwombeni ushauri Mwenyezi Mungu, tabarakuni kwa wepesi, kuweni karibu na walio wanunu<sup>28</sup>, jipambeni kwa upole, acheni viapo, acheni uongo na acheni dhuluma, wafanyieni wadhulumiwa insafu msiikaribie riba, tekelezeni vipimo na mzani, msiwapuguzie watu vitu vyao wala msiwe wafisadi katika ardhi”<sup>29</sup>

Na katika riwaya nyingine imeelezwa kwamba aliingia sokoni akawakuta watu wakiuza na wengine wakinunua akalia kilio kikubwa kisha akasema: “Enyi watumwa wa dunia na wafanyakazi wake, mkiwa mchana mnaapa, na usiku mnalala juu ya vitanda vyenu, na kutokana na hilo mnasahau akhera, wakati gani mtaandaa masurufu yenu na mkafikiria Qiyama.”

Mtu mmoja akamwambia: Ewe Amirul-Mu’mnin ni lazima watu waishi tufanyeje? Akasema: “Hakika kutafuta maisha kwa halali haimzui yeye kufanya kwa ajili ya akhera, na iwapo utasema hapana budi kulimbikiza mali hautakuwa na udhuru.”<sup>29</sup>

Hivyo ndivyo Amirul-Mu’mnin {a.s} anavyotufundisha matendo yetu yawe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu {a.j} na nafsi zetu zisifungamane na sababu pekee.

Hivyo ndivyo anavyotaka Amirul-Mu’mnin {a.s} katika serikali yake ya kiislamu na katika miji mingine ya kiislamu soko liwe mahali pa amani kwa anayeingia humo, na wala asifanyiwe udanganyifu wa wafanya vitimbi, na neema ilijoje ya adabu ambazo Amirul-Mu’mnin {a.s} amewafundisha wafuasi wake.

<sup>27</sup> *Kaafi*, Juz. 5, uk. 151.

<sup>28</sup> *Kaafi*, Juz. 5, uk. 151.

<sup>29</sup> *Mizanul-Hikma*, Hadithi 9046.

## Adabu za Sokoni na Njiani

### ADABU ZA MNUNUZI

Zipo aina mbili za watu ambao wanakusudia kwenda sokoni:  
Mosi: Mwenye kukusudia kwa haja yake kama vile anakusudia kununua mahitaji mbalimbali au kumuona humo mmoja wao.

Pili: Mwenye kukusudia kwa ajili ya kazi, kama vile ana duka humo au mkokoteni anauzia kwa huo, kwa hivyo aina zote mbili hizi zina adabu maaalum ambazo tutazieleza punde, kwanza tutaeleza adabu za mwenye kukusudia kwenda sokoni kwa kuwa ana mahitaji humo.

### KUAMINI SOKO LA WAISLAMU

Ni juu ya kila mwislamu kuliamini soko la waislamu, wala asiulize kila kitu kinachotolewa na kuingizwa humo je! hiki ni cha halali au cha haramu? Au kila nyama je! imechinjwa au hapana? Bali aamini soko lao na ajengee kwamba kila kitu kilichopo humo kuwa ni cha halali, na zime-pokewa hadithi chungu nzima zenye kutilia mkazo juu ya mchakato huo.

Mtu mmoja alimuuliza Imam Swadiq {a.s} kwa kusema: “Sisi tunanunua khufu sokoni kwetu basi waonaje katika swala kwayo?” Imam {a.s} akasema: “Swali nayo mpaka wakwambie kuwa inatokana na mzoga kwa dhati yake.”<sup>30</sup>

Imepokewa kutoka kwa Imam Abu Hasan {a.s} alipoulizwa na mmoja wao akisema: “Naingia sokoni na ninanua khufu na sijui kama inatokana na kilichochinjwa au hapana?” Akamwambia: “Swali nayo...” Muulizaji akamwambia: “Mimi sina raha kwa hili.” Imam {a.s} akamwambia: “Je! Waacha yale aliyokuwa akiyafanya Abul Hasan?”<sup>31</sup> Na pindi muulizaji

<sup>30</sup> *Kaafi*, Juz. 3, uk. 403.

<sup>31</sup> *Kaafi*, Juz. 3, uk. 404.

## **Adabu za Sokoni na Njiani**

alipomwambia Imam {a.s}: “Hakika mimi sioni raha kwa hilo.” alikuwa anamaanisha kwamba nafsi yake haina raha isipokuwa kwa kuwekewa mkazo kwamba hiyo imechinjwa.

Na Imam akamjibu kwa jawabu la kukata shauri: “Si wajibu kwako kuuliza”.

Na huenda katika hadithi hii ni ponyo kwa yule ambaye hupatwa na wasi wasi katika mambo yake.

Na katika hali yoyote ile uaminifu wa soko la waislamu humsahilishia aliyefikia umri wa balehe, na suala hili linapelekea kupatikana utulivu katika nafsi ya muumini kutokana na chanzo cha riziki yake ni chanzo cha kweli na chenye kuaminiwa kwake.

## **UTAAMILIANA NA NANI SOKONI?**

Kwa kuwa soko ni mahala ambapo hukusanyika waletaji wa biashara humo, ni hali ya kawaida tabia zao ziwe nyingi na zitofautiane, kuanzia ada zao hadi tabia zao, kwa hivyo inampasa mwingiaji sokoni kwa lengo la kununua amchunguze yule anayetaka aamiliane naye ili asifikwe na mdan-ganyifu, mpunguzaji au mwizi.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Swadiq {a.s} ambaye ni mionganoni mwa Ahlul-Bayt {a.s} amesema: “Msichanganyike wala usiamiliane isipokuwa na yule aliyekulia katika kheri.”<sup>32</sup>

---

<sup>32</sup> *Kaafi*, Juz. 5, uk. 159.

## Adabu za Sokoni na Njiani

Hadithi hii inatufundisha kwamba tusiruhusu haraka na ufinyu wa wakati ukatupelekea tukanunua kwa muuzaji yeyote, bali tununue kwa wauzaji tunaojua nyendo zao kuwa ziko sawasawa, na kwa hivyo hatutafikwa na yale tuliyoyataja miongoni mwa mambo kama vile wizi, udanganyifu, utapeli, ulimbikizaji au wauzaji ghali.

## KUMTAJA MWENYEZI MUNGU SOKONI

Zimepokewa hadithi nyingi kuhusiana na mambo ya mustahabu na dhikiri anazozisoma mtu sokoni, wakati wa kununua na kuangalia bidhaa, na hapa tunazitaja dhikiri hizo kama ifuatavyo:

## DHIKRI WAKATI WA KUINGIA SOKONI

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Swadiq {a.s} amesema:

“Unapoingia sokoni sema:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ عَدْدُ مَا يَنْطَقُونَ سُبْحَانَ اللَّهِ عَدْدُ مَا يَسْوُمُونَ تَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ  
"الْخَالِقُونَ"

mara tatu kisha sema:<sup>33</sup>

"سُبْحَانَ اللَّهِ عَدْدُ مَا يَبْغُونَ سُبْحَانَ اللَّهِ عَدْدُ مَا يَنْطَقُونَ سُبْحَانَ اللَّهِ  
عَدْدُ مَا يَسْوُمُونَ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ" <sup>1</sup>

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Baqir {a.s} amesema: “Mwenye kuingia sokoni na akaangalia vitu vyake vitamu, na vichungu vyake na vya uchachu wake basi aseme:

أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُ  
اللَّهِ أَنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ وَأَسْتَجِيرُ بِكَ مِنْ الظُّلْمِ وَالْغَرْمِ وَالْمَأْثَمِ"

“Nashuhudia hakuna Mungu anayestahiki kuabudiwa isipokuwa

<sup>33</sup>. Usuul Sitta Ashara uk. 114.

## Adabu za Sokoni na Njiani

Mwenyezi Mungu wapekee hana mshirika, na hakika Muhammad ni mja wake na mjumbe wake, Ee Mola wangu hakika mimi nakuomba kwa fadhila zako uniepushe na dhulma, hasara na dhambi”<sup>34</sup>

Imepokewa hadithi nyingine kutoka kwa Imam Swadiq {a.s} amesema: “Mwenye kusoma sokoni:

اَشَهَدُ اَنْ لَا إِلَهَ اِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشَهَدُ اَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ  
وَرَسُولُهُ كَتَبَ اللَّهُ لَهُ الْأَفْلَافَ حَسَنَةً”

Mwenyezi Mungu atamwandikia yeye maelfu ya mema”<sup>35</sup>

## DHIKRI WAKATI WA KUNUNUA:

Na imepokewa hadithi kutoka kwa mmoja kati ya hao wawili yaani Imam Baqir {a.s} au Imam Swadiq {a.s} amesema: “Utakaponunua bidhaa basi sema: *Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar*, kisha sema:

اَللَّهُمَّ اِنِّي اشْتَرَيْتُهُ التَّمَسُّ فِيهِ مِنْ خَيْرِكَ فَاجْعَلْ لِي فِيهِ خَيْرًا اللَّهُمَّ  
اِنِّي اشْتَرَيْتُهُ التَّمَسُّ فِيهِ مِنْ فَضْلِكَ فَاجْعَلْ لِي فِيهِ فَضْلًا اللَّهُمَّ اِنِّي  
اشْتَرَيْتُهُ التَّمَسُّ فِيهِ مِنْ رِزْقِكَ فَاجْعَلْ لِي فِيهِ رِزْقًا”

“Ee Mola wangu hakika mimi nimenunua nategemea heri zako basi nijaalie heri kwayo, Ee Mola wangu hakika mimi nimenunua nategemea fadhila zako basi nipe fadhila kwayo, Ee Mola wangu hakika mimi nimenunua nategemea riziki yako basi niruzuku kwayo”<sup>36</sup>

Na katika hadithi ya Imam Ali Ridha {a.s}: “Alikuwa akiandika katika mzigo *Barakatul-lana*”<sup>37</sup>

<sup>34</sup>. Mahasin juz. 1 uk. 40.

<sup>35</sup> *Mahasin* Juz. 1 uk. 40.

<sup>36</sup>. *Man la Yahdhuruhul-Faqiih* juz. 3 uk. 200.

<sup>37</sup> *Man la Yahdhuruhul-Faqiih* Juz. 3 uk. 201.

## Adabu za Sokoni na Njiani

### KUWEKA MIPAKA YALE UNAYONUNUA

Hakika hadithi zilizopokewa kutoka kwa bwana Mtume {s.a.w.w} na Ahlul-Bayt {a.s} zimetaja suala muhimu, nalo mtu asinunue bidhaa bila kipimo, asimwambie hivi: “Niuzie hii katika mfuko huu.” yaani kwa kiwango kilichomo, bali ni lazima amjulishe kiwango chake.

Imepokewa hadithi kutoka kwa bwana Mtume {s.a.w.w} amesema: “Pimeni vyakula vyenu, hakika chakula kinachopimwa kina baraka nyin-gi.”<sup>38</sup>

### MUUZAJI SOKONI

Hakika kazi za sokoni zina mema mengi sana kwa sababu kazi hiyo huh-esabiwa kuwa ni kufanya biashara, na kufanya biashara ni sunna, na soko ni kimbilio la mafukara pindi maisha yanapokuwa magumu na nafasi za kazi zinapokuwa chache.

Kwa hakika Maimamu wetu waliwaamrisha baadhi ya wafuasi wao pindi maisha yanapokuwa kwao magumu wajishighulische sokoni katika yale ambayo anayoyeridhia Mwenyezi Mungu {a.j}.

Imekuja katika hadithi kwamba mmoja wao alimwambia Imam Swadiq {a.s}: Nilikuwa na kitu mkononi mwangu lakini nikakikosa na maisha yakaniwiwa magumu sana. Imam {a.s} akamuuliza: “Je! Unalo duka sokoni?” Akasema: Ndiyo. Akasema {a.s}: “Utakaporejea kwenye mji wa Kufa basi kakae dukani kwako...”<sup>39</sup> Kwa hivyo lipo katazo kwa yule ambaye anayemiliki biashara au duka kisha akaliacha au akaacha kufanya biashara.

<sup>38</sup> *Mizanul-Hikma*, Hadithi 2051.

<sup>39</sup> *Kaafi*, Juz. 3, uk. 474.

## Adabu za Sokoni na Njiani

Ipo hadithi iliyopokewa kutoka kwa Imam Swadiq {a.s} kwamba nilimwambia yeye: "Mimi nimeazimia kuacha kujishughulisha sokoni na ninacho kitu mkononi mwangu." Imam {a.s} akasema: "Kwa hivyo inapoanguka rai yako hakitakusaidia wewe chochote."<sup>40</sup>

Kwa hivyo soko ni sehemu ya kukutana watu na kujuana juu ya rai zao na maelekezo na mitazamo yao mbalimbali kwa ajili ya kupata uzoefu na kufaidika kutokana na biashara zao, kwa hakika ni shule ya kivitendo.

## MAHALA PA KUUZA SOKONI

Mara nyingi tunawaona wauzaji wengi wakizozana kuhusiana na sehemu ya kuuzia, kwani kila mmoja hudai sehemu fulani ni mahala pake, na kwamba alikuwa anauza hapo kabla ya kutokea mzozo, au anakuwa mmoja wao amezoea kuweka mkokoteni wake sehemu fulani kisha anakuja kumkuta muuzaji mwingine ameweka mkokoteni wake katika sehemu yake, basi hapo watatofautiana kuhusu ni nani mwenye haki zaidi ya mahala hapo, na kila mmoja anadai na kumtuhumu mwenzake kuwa amepora sehemu hiyo.

Na lau tutazirejea hadithi za Ahlul-Bayt {a.s} tunazikuta zinaeleza kwamba mwenye kutangulia katika sehemu fulani basi yeye ana haki zaidi.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Amirul-Mu'minin {a.s} amesema: "Soko la waislamu ni kama vile msikiti wao, mwenye kutangulia sehemu basi yeye ana haki zaidi hadi usiku."<sup>41</sup>

---

<sup>40</sup> *Kaafi*, Juz. 5, uk. 149.

<sup>41</sup> *Kaafi*, Juz. 3, uk. 662.

## Adabu za Sokoni na Njiani

### ADABU ZA MUUZAJI

Tutazitaja baadhi ya adabu ambazo hapana budi ajipambe nazo yule anayejishughulisha sokoni.

Zipo hadithi mbalimbali za Ahlul-Bayt {a.s}, Maasumu na Watoharifu zinazoelezea adabu, nazo ni:

#### 1. DUA SOKONI

Zipo baadhi ya dua ambazo ni mustahabu, ambazo zinasomwa sokoni hasa hasa kwa muuzaji, mionganoni mwa dua hizo ni:

##### i. Wakati wa kutoka Sokoni:

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Swadiq {a.s} amesema: "Utapotaka kutoka kwenda sokoni kwako, basi swali rakaa mbili au nne, kisha baada ya swala sema hivi:

"تَوَجَّهْتُ بِلَا حَوْلٍ وَلَا قُوَّةٍ إِلَّا بِكَ فَأَنْتَ حَوْلِي وَمَنْكَ قُوَّةٌ إِلَّا بِكَ فَارْزَقْنِي مِنْ فَضْلِكَ  
الْوَاسِعِ رِزْقًا كَثِيرًا طَيِّبًا وَأَنَا خَافِضٌ فِي عَفْيِكَ فَإِنَّهُ لَا يَمْلِكُهَا أَحَدٌ  
غَيْرُكَ"

"Nimeelekea bila ya ustadi kutoka kwangu wala nguvu, lakini ni kwa ustadi wako na nguvu zako, najiepusha kwako- nijidhaniye - kuwa nina ustadi na nguvu, ila kutoka kwako, Wewe ndio ustadi wangu, na nguvu zangu ni kutoka kwako. Ewe Mungu wangu, niruzuku kutokana na fadhila zako zenye wasaa riziki nyingi nzuri, na mimi nina wasaa katika afya yako, kwa kuwa haimiliki yejote asiyekuwa wewe."<sup>42</sup>

<sup>42</sup>. Kaafi juz. 3 uk. 474.

## Adabu za Sokoni na Njiani

---

### ii. Wakati wa kuingia Sokoni:

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Baqir {a.s} amesema: “Hakuna mtu muumini anayekwenda au anakuja katika kikao chake au sokoni kwake na akasema pindi anapoweka mguu wake sokoni:

**اللَّهُمَّ أَنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ خَيْرِهَا وَخَيْرِ أَهْلِهَا** “Ee Mungu wangu hakika mimi ninakuomba kutokana na kheri zake na kheri za watu wake” isipokuwa Mwenyezi Mungu humtumia mwenye kumuhifadhi na atahifadhika hadi atakaporejea nyumbani kwake, na atamwambia yeye: “Hakika siku hii ya leo umekingwa na shari za soko na shari za watu wake kwa idhini ya Mwenyezi Mungu {a.j} na umeruzukiwa heri zake na heri za watu wake katika siku hii...”

### iii. Wakati wa kukaa katika sehemu ya biashara:

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Baqir {a.s} amesema: “... na atakapokaa katika sehemu yake aseme:

**"أَشْهُدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ وَأَشْهُدُ أَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ اللَّهُمَّ أَنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ حَلَالًا طَيْبًا وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ صَفْقَةٍ حَاسِرَةٍ وَيَمِينَ كاذِبَةٍ"**

“Nashuhudia hakuna Mungu anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu wapekee wala hana mshirika, na ninashuhudia Muhammad ni mja wake na mjumbe wake, Ee Mungu wangu hakika mimi nakuomba kutokana na fadhila zako halali nzuri, na najilinda kwako kutokana na kupata hasara na kiapo cha uwongo” na atakaposema hivyo Malaika aliyetumwa kwa ajili yake atamwambia: Natoa bishara njema katika yale yaliyomo katika soko lako hakuna mtu ye yeyote mwenye hadhi kubwa zaidi yako, hakika imeleta mema haraka na kufuta mabaya, na yatakujia yale ambayo Mwenyezi Mungu amekugawia, halali iliyokithiri na nzuri na yenye baraka humo”<sup>43</sup>

---

<sup>43</sup> *Kaafî*, Juz. 5, uk. 155.

## Adabu za Sokoni na Njiani

---

### **2. UWAZI KATIKA KUUZA NA KUNUNUA**

Lengo la mchakato huu ni kwamba ili mtu asije kuangukia katika maasi ya Mwenyezi Mungu {a.j} kwa kuwafanyia udanganyifu waumini au muuzaji kuwafanyia hila wanunuzi, kwa hivyo inapaswa mambo kuwa wazi wakati wa uuzaji bidhaa na thamani, aidha iwepo bidhaa na vinginevyo...

Kwa hivyo imekuja katika baadhi ya hadithi ambazo zinakataza utaratibu fulani ambao huenda ukamwingiza mnunuzi katika kutapeliwa na udanganyifu, kama vile mtu anauza bidhaa yake katika kivuli au giza.

Imepokewa hadithi kutoka kwa Imam Kadhim {a.s} amesema: “Ewe Hisham hakika uuzaji wa bidhaa gizani ni udanganyifu, na hakika udanganyifu sio halali.”<sup>44</sup>

Vivyo hivyo zinamkataza muuzaji ambaye hafanyi vizuri biashara kukaa sokoni kwa ajili ya kufanya biashara . Imekuja katika hadithi kutoka kwa Amirul-Mu’minin {a.s} amesema: “Asikae sokoni isipokuwa yule ambaye ana akili ya kuuza na kununua.”<sup>45</sup>

### **3. BIASHARA ISIMPUMBAZE MTU KUHUSIANA NA SWALA**

Hakika tumeeleza hapo kabla kuhusiana na adabu za kijumla za sokoni kwamba Amirul-Mu’minin aliwalilia watu wa sokoni ambao wanjishughulisha na dunia na hali ya kusahau akhera, kwa hivyo ni juu ya kila mwenye kujishughulisha na kazi ya sokoni asisahau wakati wa swala unapoingia, bali aache kila kazi iliyopo mkononi kwake aitikie wito wa Mwenyezi Mungu {*hayya’ala swalaa*} na ajihadhari kwa hadhari yote usemajji wa baadaye wa kishetani kwamba wakati ni mrefu kwa hivyo

---

<sup>44</sup> *Kaafi*, Juz. 5, hadithi 161.

<sup>45</sup> *Kaafi*, Juz. 5, uk. 154.


## Adabu za Sokoni na Njiani

nitaswali baada ya muda kidogo baada ya kuondoka wanunuzi, kwani hilo ni mionganini mwa mbinu zake zenye kuhadaa mpaka usahau wito wa Mwenyezi Mungu, au kukukosesha fadhila ya swala katika wakati wake.

Imepokewa katika hadithi tukufu kwamba mmoja wao alimwambia Imam Ridha {a.s}: Mimi nakuwa sokoni na ninajua wakati na inaniwia vifinyu kwangu kuingia na kuswali, akasema: “Hakika Shetani ana ukaribu na jua katika hali tatu: Ikiwa mwanzoni, katikati na litakapozama, basi swalii baada ya kupinduka jua hakika shetani anataka akuingize katika upanga utakaokukata na kumwacha mwengine.”<sup>46</sup>

## KUTOAPA KATIKA BIASHARA

Mwenyezi Mungu {a.j}



“Wala msimfanye Mwenyezi Mungu ni kizuizi cha viapo vyenu...”  
2:224

Hakuna shaka kwamba kiapo cha uongo ni haramu katika sheria na bila kutegemea huenda akafanya binadamu muumini mfano wa matendo hayo ya haramu na mabaya, lakini ni nini kiapo cha kweli? Je! binadamu anawenza kuapa katika mambo ya kibiashara iwapo atakuwa mkweli katika maneno yake?

Hakika Qur’ani tukufu inatukataza kuapa hata kama tukiwa wakweli, na Ahlul-Bayt {a.s} wakatilia mkazo na kusisitiza kuwa ni makuruju kufanya hivyo.

<sup>46</sup> *Kaafi*, Juz. 3, uk. 290.

## Adabu za Sokoni na Njiani

Imepokewa hadithi kutoka kwa Amirul-Mu'minin {a.s} amesema: "Enyi wafanyabiashara, jiepusheni na vitu vitano; Usifiaji wa muuzaji, dharau ya mnunuzi, kiapo katika kuuza, kuficha aibu na riba, halali kwenu itakuwa sahihi na mtaepukana na haramu."<sup>47</sup>

Na imepokewa hadithi kutoka kwa Amirul-Mu'minin {a.s} amesema: "Ole wenu na kuapa, kwani kiapo hutia kipato katika biashara na hufuta baraka."<sup>48</sup>

Na imepokewa hadithi kutoka kwa Mtume {s.a.w.w} amesema: "Mambo manne mwenye kuwa nayo kitakuwa kizuri kichumo chake, ikiwa atanunua bila kutia kasoro, na atakapouza hasifii, wala hafanyi udanganyifu na kati ya hayo haapi."<sup>49</sup>

<sup>47</sup> *Wasa'il Shi'ah*, Juz. 12 uk. 284 cahpa ya Daru Ihya Turaath Arabi, Juzu 20.

<sup>48</sup> *Kaafi*, Juz. 5, uk. 162.

<sup>49</sup> *Miizanul-Hikma*, Hadithi 2038.

## Adabu za Sokoni na Njiani

### ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza mpaka Ishirini na Nne
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhang'a wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.

## Adabu za Sokoni na Njiani

29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeesi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba' Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'an na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekeea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza

## Adabu za Sokoni na Njiani

62. Nahju'l-Balaghah - Juzuuy ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Tujifunze Misingi Ya Dini
68. Sala ni Nguzo ya Dini
69. Mikesha Ya Peshawar
70. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
71. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
72. Shia asema haya, Sunni asema haya, Wewe wasemaje?
73. Liqaa-u-llaah
74. Muhammad (s) Mtume wa Allah
75. Amani na Jihadi Katika Uislamu
76. Uislamu Ulienea Vipi?
77. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
78. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
79. Urejeo (al-Raja'a )
80. Shahidi kwa ajili ya Ubinadamu
81. Utokezo (al - Badau)
82. Kuanzia ndoa hadi kuwa wazazi
83. Myahudi wa Kimataifa
84. Uislamu na dhana
85. Mtoto mwema
86. Johari za hekima kwa vijana
87. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
88. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
89. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
90. Tawasali
91. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
92. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu

## Adabu za Sokoni na Njiani

93. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
94. Swala ya maiti na kumlilia maiti
95. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
96. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
97. Hadithi ya Thaqlain
98. Fatima al-Zahra
99. Tabaruku
100. Sunan an-Nabii
101. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
102. Idil Ghadiri
103. Mahdi katika sunna
104. Kusalia Nabii (s.a.w)
105. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
106. Ujumbe - Sehemu ya Pili
107. Ujumbe - Sehemu ya Tatoo
108. Ujumbe - Sehemu ya Nne
109. Shiya N'abasahaba
110. Iduwa ya Kumayili
112. Maarifa ya Kiislamu.
113. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
114. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
115. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano

## Adabu za Sokoni na Njiani

### BACK COVER

Sehemu za Umma wa Kiislamu ambazo watu wote hushirikiana katika Uislamu zina hukumu na adabu zake, hivyo, ni juu ya kila binadamu mwenye imani kuzichunga na kutokwenda kinyume nazo. Mtu hana haki yoyote ya kujipendelea na kuzitumia kwa ajili yake binafsi, na sio milki ya mtu fulani, kuwa yeche ndiye anayestahiki na kujilimbikizia yeye, au azitumie namna apendavyo, mfano wa sehemu hizo ni njia na soko. Kwa hakika, watu wote wana haki sawa katika utumiaji wa vitu hivyo, kwa hivyo, hapa linakuja swali: Ni adabu na desturi zipi ambazo Uislamu umeziweka kuhusiana na sehemu hizo na ambazo umetutaka sisi tuzifuate?

Inafahamika vizuri kwamba kwa vile Uislamu ni dini na ni mfumo wa maisha, hivyo, haukuacha jambo lolote linahusu maisha ya mwanadamu. Uislamu umetengeneza kanuni, sheria na adabu zinazohusu kila suala la mwanadamu. Soko na njia ni maeneo ambayo watu wa kila aina huyatumia katika maisha yao ya kila siku. Katika muktadha huu, soko ni kuanzia maduka madogo ya mitaani, maduka makubwa (*supermarkets*), na masoko ya kitaifa na kimataifa. Njia katika muktadha huu ni kuanzia njia za kawaida wanazotumia watu (za miguu), barabara za magari, reli, usafiri wa majini na angani, kitaifa na kimataifa. Kwa hiyo, Uislamu umeweka kanuni, sheria na adabu kwa ajili ya matumizi ya watu katika maeneo hayo ili kulinda haki ya kila mtu.

Mwandishi wa kitabu hiki ameellezea kanuni, sheria na adabu zinazotumika katika maeneo hayo kwa mujibu wa mafundisho ya Kiiislamu ambayo ni kutoka katika Qur'ani Tukufu na Sunna.

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: [alitrah@raha.com](mailto:alitrah@raha.com)

Tovuti: [www.alitrah.org](http://www.alitrah.org)

Katika mtandao: [www.alitrah.info](http://www.alitrah.info)